

NATIONAL ASSEMBLY LIBRARY  
ACC 7500

**THE KENYA AFRICAN NATIONAL UNION  
(KANU)**

PARLIAMENT  
OF KENYA  
LIBRARY




**Nomination Rules**

Price: KSh. 10/-

18 FEB 1988

KENYA AFRICAN NATIONAL UNION  
(KANU)



# Nomination Rules

KENYA NATIONAL ASSEMBLY

Accession: 10013546

Call No: 324.267 621 KAN



001

002

003

NATIONAL ASSEMBLY LIBRARY

ACCESSION No. 3

LOCATION \_\_\_\_\_

THE KENYA AFRICAN NATIONAL UNION (KANU)  
NOMINATION RULES

**ARRANGEMENT OF RULES**

**Part I: Introduction and interpretation**

1. Short title.
2. Interpretation.
3. Application.
4. Amendments.

**Part II: Appointment of officers**

5. Returning officers.
6. Presiding officers.
7. Nomination officers.

**Part III: Commencement of nomination procedures**

8. Application for party clearance.
9. Verification of eligibility.
10. Ratification of list of eligible applicants.
11. Publication of list of eligible applicants.
12. Inspection of list of eligible applicants.
13. Appeals.

**Part IV: Presentation of candidates to returning officers**

14. Date and manner of presentation.
15. Candidates not presenting themselves.

16. Compilation of the register of candidates.
17. Issuance of certificate of presentation.

**Part V: Presentation of candidates to presiding officers**

18. Date of presentation for nomination.
19. Manner of presentation for nomination.
20. Submission of documents.

**Part VI: Eligibility of Voters and Voting Procedure**

21. Eligible voters.
22. Voting procedure.

**Part VII: Processing of Votes**

23. Manner of processing votes.
24. General duty of presiding officers.
25. Special duties of presiding officers.
26. Sealing of returns.
27. Objections to returns or sealing.
28. Dispersal of voters.

**Part VIII: Declaration of results and nomination**

29. Compilation of votes by returning officers.
30. Declaration of results.
31. Declaration of nominated candidates.

**Part IX: Finances**

32. Financial matters.

**Part X: General**

33. The power to issue orders.

18 FEB 1988

# THE KENYA AFRICAN NATIONAL UNION (KANU) NOMINATION RULES

Art. 22

## Part I: Introductory and Interpretation

1. The Rules may be cited as the Kenya African National Union (KANU) Nomination Rules (hereinafter the Rules).

2. In these Rules, unless the context otherwise requires—  
“agent” means a person duly accredited by a candidate as his agent;

“candidate” means a person who has been cleared by the Party in accordance with Part III of these Rules;

“election” or “elections” means an election or elections referred to in rule 3 herein;

“nomination officials” means persons appointed in accordance with and for purposes of rule 7 herein or any other person officially engaged in the nomination process;

“party” means the Kenya African National Union (KANU);

“polling station” means any place set aside for voting in accordance with these Rules;

“presiding officer” means a person appointed or designated under these Rules to preside at a polling station;

“register” means a register of candidates compiled in accordance with rule 16 herein.

“returning officer” means a person designated under these Rules to conduct nominations in his respective area of jurisdiction.

“voter” means any person who is validly registered as a Party member and is in possession of a current membership card; and

“voting” means the act of expressing preference in favour of a candidate in accordance with rule 21 herein and cognate expressions shall be construed accordingly.

3. The Rules shall govern nomination of Party candidates in respect of any election to be held under the National Assembly

and Presidential Elections Act (Cap. 7) and the Local Government Elections Act (Cap. 265).

4. These Rules may be amended from time to time with the approval of the Governing Council.

### **Part II: Appointment of Officers**

5. The Provincial Commissioner, Nairobi Province and district commissioners shall be the returning officers in their respective areas of jurisdiction.

6. The returning officer shall, in respect of each polling station in his area of jurisdiction, appoint a presiding officer.

7. The returning officer may further appoint other nomination officials to assist in matters pertaining to Party nominations.

### **Part III: Commencement of Nomination Procedures**

8. All persons seeking clearance/nomination of KANU in respect of any election for which these Rules apply shall submit to the President of the Party a duly completed *Pledge of Loyalty* form obtainable from the Party headquarters.

9. The Party National Executive Committee shall compile the list of names received in accordance with rule 8 and shall satisfy itself of the eligibility of each person for Party clearance/nomination in accordance with the provisions of the Party Constitution.

10. The list of all applicants together with the comments of the National Executive Committee shall be submitted to the Party National Governing Council for approval.

11. Upon approval, the Party shall compile and publish the list of names of all persons who have been cleared by the Party in at least one newspaper circulating throughout Kenya, and in addition copies thereof shall be sent to the Office of the President, the Supervisor of Elections, the Director of Local Government Elections and all returning officers.

12. The list compiled and published under rule 11 shall be open for inspection at the offices of returning officers by all persons interested in the Party nomination for a period of three days after its publication.

13. Any person who considers that his name has been inadvertently, wrongly or unfairly omitted from that list shall have the right to appeal to the Party President within a period of four days after the expiry of the inspection period.

#### **Part IV: Presentation of Candidates to Returning Officers**

14. Upon a day and time or times to be specified by the Party President, all candidates shall present themselves before their respective returning officers with the following items:

- (a) A national identity card.
- (b) The Party life membership certificate.
- (c) A voter's registration card.
- (d) A non-refundable Party sponsorship fee of KSh. 1,500 for Local Government and KSh. 3,000 for National Assembly election candidates.

15. Any candidate who fails to present himself on the day and at the time and place specified in accordance with rule 14 shall be disqualified from nomination.

16. Returning officer shall compile a register of all those who have presented themselves before him and shall distribute a copy thereof to the Office of the President, KANU headquarters, the Supervisor of Elections, the Director of Local Government Elections and all presiding officers under his jurisdiction.

17. All candidates appearing in the register compiled under rule 16 shall be issued with a certificate in the form attached to these Rules, signed by the returning officer confirming that they have satisfied all the requirements for nomination.

#### **Part V: Presentation of Candidates to Presiding Officers**

18. Not later than twenty-one days before any election referred to in rule 3 is held, the Party President shall designate a day upon which all candidates appearing in the register shall present themselves before the presiding officers for nomination.

19. On the designated day each candidate shall present himself either in person or through duly accredited agent at each designated polling station in the constituency/ward in which he wishes to stand for elections.

20. Each candidate or his duly accredited agents shall submit the following documents to the presiding officer of each polling station:

- (a) The certificate or a copy thereof issued by the returning officer under rule 17.
- (b) A valid Party membership card.
- (c) A national identity card.
- (d) A voter's registration card bearing the name of the relevant constituency/ward.

#### **Part VI: Eligibility of Voters and Voting Procedure**

21. All paid up KANU members who are not under suspension from the Party or are otherwise disqualified from voting under Caps. 7 and 265 aforesaid, shall be entitled to express their preference by lining up behind the candidate of their choice or in his absence, behind his duly accredited agent.

22. At each polling station the following rules shall apply:

- (a) Polling stations shall be clearly marked by the presiding officer.
- (b) Voting in respect of candidates seeking election to the National Assembly shall commence at 12.00 noon on the day designated under rule 18 and shall continue until the presiding officer has processed all the votes in accordance with part VII herein.
- (c) Voting in respect of candidates seeking election to local authorities shall commence immediately after votes for National Assembly candidates have been processed and shall continue until the presiding officer has processed all the votes in accordance with part VII herein.
- (d) There shall be no campaigning whatsoever within the vicinity of polling stations.
- (e) Except for the returning officer, presiding officer, nomination officials and accredited agents, persons not registered as voters in a given polling station shall not be allowed to enter into or vote in that station, nor will such persons be permitted to remain within a radius of one hundred yards thereof.

- (f) All duly accredited agents, a list whereof shall be provided to the presiding officer, shall carry a black and white portrait measuring approximately 16"×24" of the candidate they are representing.
- (g) All voters shall hold their KANU membership cards in such a manner as to display the Party stamps clearly affixed thereon.
- (h) Voters shall remain orderly and in a straight line throughout the voting.
- (i) No voter once in line shall be permitted to cross over to another line after the processing of votes has commenced in accordance with Part VIII herein.
- (j) All voters shall identify themselves by producing a valid voter's registration card for the registration area.

### **Part VII: Processing of Votes**

23. Voting at each polling station shall be processed by adding up the total number of voters behind each candidate or his duly accredited agent at that station.

24. The presiding officer and nomination officials shall ensure that the processing of votes in accordance with rule 23 is done in an orderly, accurate and responsible manner.

25. Notwithstanding the generality of rule 24, the presiding officer shall—

- (a) deal fairly with all complaints and other matters put to him by the candidates or their duly accredited agents;
- (b) process the votes by counting the voters in each line in a loud and audible voice;
- (c) record the total number of voters in each line on a certificate which shall be countersigned by the candidate or his duly accredited agent; and
- (d) supply each candidate or his duly accredited agent with a copy of the certificate referred to in (c) above.

26. As soon as all votes have been processed in the manner specified in rules 23 to 25 above, the presiding officers shall

submit all returns from each polling station under their charge, duly sealed in the presence of all candidates or their duly accredited agents, to their respective returning officers.

27. In the event that any candidate or his duly accredited agent refuses to countersign the certificate of results or object to the manner in which the returns are sealed, the presiding officer shall record that fact and the reasons tendered in respect thereof and submit the same together with the returns to the returning officer.

28. All voters shall disperse as soon as the processing of votes in accordance with this part has been completed.

### **Part VIII: Declaration of Results and Nomination**

29. On receipt of returns from all presiding officers under his charge, the returning officer shall in the presence of all candidates or their duly accredited agents compile the total number of votes recorded in respect of each constituency/ward.

30. The returning officer shall immediately thereafter declare the results obtained from each constituency/ward by declaring the total number of votes recorded in respect thereof and the number of such votes recorded in favour of each candidate.

31. (i) Any candidate who has presented himself without opposition at all polling stations in his constituency/ward in the manner specified in part V of these Rules or obtains more than 70 per cent of the total votes recorded in each constituency/ward shall without any further assurance be declared nominated by the Party as the sole candidate to stand for elections in that constituency/ward in accordance with the provisions of the National Assembly and Presidential Elections Act, or the Local Government Act, aforesaid.

(ii) Any candidate who—

(a) obtains at least 30 per cent of the total number of votes recorded in each constituency/ward; or

(b) is among the top three contestants in any constituency/ward in circumstances where no candidate qualifies under (i) above or less than three candidates qualify under (a) herein.

shall without any further assurance, be declared nominated by the Party to stand for elections in that constituency/ward in accordance with the provisions of the National Assembly and Presidential Elections Act, or the Local Government Act, aforesaid.

(iii) Any candidate who fails to obtain nomination as stipulated above may, if he is dissatisfied with the decision of the returning officer, appeal to the Party President within twenty-four hours thereof and the President shall have power to vary that decision as he deems fit.

#### **Part IX: Finances**

32. KANU shall meet all operational costs of the nomination process including printing, supervision, the provision of materials and allowances for nomination officials.

#### **Part X: General**

33. The Party President may issue orders for the better carrying into effect of these Rules and without prejudice to the generality of the foregoing, orders issued under this rule may make provision for—

- (a) the gazettelement or notification of designated polling stations;
- (b) the procedure for appeals under rule 13;
- (c) the procedure and conduct of voting at designated polling stations;
- (d) the scale of remuneration of nomination officials;
- (e) specifying anything to be specified under these Rules.

**CERTIFICATE OF PRESENTATION**

*(Under Rule 17)*

This is to certify that:

.....

bearer of ID Card No. ....

Party Life Membership Certificate No. ....

Voter's Registration Card No. ....

has met all the requirements for presentation to voters for Party nomination in

..... constituency/ward.

Signed .....

*Returning Officer*

..... District

**KANUNI ZA UTEUZI ZA KANU**  
**(THE KENYA AFRICAN NATIONAL UNION)**

**MPANGO WA KANUNI**

**Sehemu ya Kwanza: Utangulizi na Maelezo**

1. Jina fupi.
2. Maelezo.
3. Namna kanuni zitakavyotumika.
4. Marekebisho.

**Sehemu ya Pili: Uteuzi wa maafisa**

5. Wasimamizi wa uchaguzi.
6. Wakuu wa vituo vya upigaji-kura.
7. Maafisa wa uteuzi.

**Sehemu ya Tatu: Kuanza kwa utaratibu wa uteuzi**

8. Maombi ya kutaka kuruhusiwa na Chama.
9. Uthibitisho wa wagombea-uchaguzi.
10. Kupitishwa orodha ya wale wanaopeleka maombi.
11. Uchapishaji wa orodha ya waombaji waliopitishwa.
12. Ukaguzi wa orodha ya waombaji waliopitishwa.
13. Ukataji rufani/kuwasilisha malalamiko.

**Sehemu ya Nne: Kujipeleka kwa wagombea-uchaguzi kwa wasimamizi wa uchaguzi**

14. Tarehe na namna ya kufika.
15. Wagombea-uchaguzi wasioweza kufika.

16. Uandishi wa rejista la wagombea-uchaguzi.
17. Kutolewa kwa cheti cha kujiwasilisha.

**Sehemu ya Tano: Kujipeleka kwa wagombea-uchaguzi kwa wakuu wa vituo vya upigaji-kura**

18. Tarehe na kujipeleka kwa ajili ya uteuzi.
19. Namna ya kuhudhuria kwa ajili ya uteuzi.
20. Kufikisha hati au nyaraka.

**Sehemu ya Sita: Uwezo wa wapigaji-kura na njia ya upigaji-kura**

21. Wapigaji-kura wenye haki ya upigaji-kura.
22. Njia ya upigaji-kura.

**Sehemu ya Saba: Kuhesabu kura kwenye vituo vya upigaji-kura**

23. Namna ya kuhesabu kura.
24. Wajibu wa jumla wa wakuu wa vituo vya upigaji-kura.
25. Wajibu maalumu wa wakuu wa vituo vya upigaji-kura.
26. Kufungwa kwa matokeo.
27. Ubishi juu ya matokeo au kufungwa kwa matokeo.
28. Watakavyotawanyika wapigaji-kura.

**Sehemu ya Nane: Utangazaji wa matokeo na uteuzi**

29. Uandishi wa jumla ya kura na wasimamizi wa uchaguzi.
30. Matangazo ya matokeo.
31. Matangazo ya wagombea-uchaguzi walioteuliwa.

**Sehemu ya Tisa: Fedha na malipo**

32. Mambo yanayohusu fedha.

**Sehemu ya Kumi: Kwa jumla**

33. Uwezo wa kutoa amri.

# KANUNI ZA UTEUZI WA KANU (THE KENYA AFRICAN NATIONAL UNION)

## Sehemu ya Kwanza: Utangulizi na Maelezo

1. Kanuni hizi zinaitwa: Kanuni za Utenzi za KANU (kila mahali katika Kanuni hizi).

2. Kwenye Kanuni hizi, isipokuwa ikielezwa vingine—

“ajenti” ni mtu ambaye amechaguliwa na mgombea uchaguzi kama mwakilishi wake;

“mgombea uchaguzi” maana yake ni mtu aliyeruhusiwa na Chama kwa kufuatana na Sehemu ya Tatu ya Kanuni hizi;

“uchaguzi” au “chaguzi” maana yake ni uchaguzi au chaguzi zilizotajwa humu chini ya kanuni nambari 3;

“maafisa uteuzi” maana yake ni watu walioandikwa kufanya kazi kwa kufuatana na kanuni nambari 7 au mtu ye yote ambaye kwa njia rasmi anashughulikia kazi inayohusiana na uteuzi;

“Chama” maana yake ni KANU (The Kenya African National Union);

“kituo cha uchaguzi” maana yake ni mahali palipotengwa kwa ajili ya upigaji-kura kwa mujibu wa Kanuni hizi;

“mkuu wa kituo cha uchaguzi” maana yake ni mtu aliyemandikwa kwa kulingana na Kanuni hizi ili kusimamia kituo cha upigaji kura;

“regista” maana yake ni orodha ya wagombea uchaguzi kwa kufuatana na kanuni nambari 16 iliyotajwa humu;

“msimamizi uchaguzi” maana yake ni mtu aliyepewa kazi chini ya Kanuni hizi kuendesha uteuzi katika eneo anakofanya kazi au eneo ambalo liko chini ya mamlaka yake;

“mpigaji kura” maana yake ni mtu ambaye jina lake limeandikishwa kama mwanachama wa Chama na ambaye anamiliki kadi ya uanachama; na

“upigaji kura” maana yake ni kitendo cha mtu kuchagua mwenyewe kwa kufuatana na kanuni nambari 21 zilizomo humu, na jinsi atakavyochagua ndivyo itakavyokubalika.

3. Kanuni hizi zitatumika kwa ajili ya shughuli zote za uteuzi zitakazofanywa kuwachagua wagombea uchaguzi wa Chama, na kuhusu uchaguzi wote wote utakaofanywa chini ya sheria (ibara nambari 7) za Uchaguzi wa Bunge na Uchaguzi wa Rais, na kuhusu sheria (ibara nambari 265) ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

#### **Sehemu ya Pili: Uteuzi wa Maafisa**

4. Kanuni hizi zinaweza kurekebisha wakati wote kwa idhini ya kamati kuu ya Chama.

5. Mkuu wa Mkoa wa Nairobi na wakuu wa wilaya watakuwa wasimamizi uchaguzi katika maeneo ambayo yamo chini ya mamlaka yao.

6. Mkuu wa uchaguzi ndiye atakayemteua mkuu wa kituo cha upigaji kura wa kila kituo cha upigaji kura katika eneo ambalo liko chini ya mamlaka yake.

7. Mkuu wa uchaguzi anaweza pia kuwateua maafisa wa uchaguzi kumsaidia yeye, na kuwasaidia wakuu wa vituo vya upigaji kura katika kazi zinazoambatana na taratibu za uteuzi wa Chama.

#### **Sehemu ya Tatu: Kuanza kwa Utaratibu wa Uteuzi**

8. Watu wote wanaotaka kuruhusiwa na KANU kwa ajili ya kusimama kwa uchaguzi wote unaohusiana na Kanuni hizi watatakiwa kuwasilisha kwa Rais wa Chama fomu iliyojazwa kikamilifu ya *Kiapo cha Utiifu*. Fomu hii inapatikana kwenye makao makuu ya Chama.

9. Kamati ya Utendaji ya Chama itaandika orodha ya majina yaliyopelekwa kwa mujibu wa kanuni nambari 8 kuhakikisha uwezo wa kila mtu aliyepeleka maombi ya kuruhusiwa na Chama kwa mujibu wa Katiba ya Chama.

10. Orodha ya waombaji wote, pamoja na mapendekezo ya Kamati ya KANU ya Utendaji, itapelekwa kwa Kamati Kuu ya Chama ili ipitishwe.

11. Baada ya orodha hiyo kupitishwa, Chama kitaiandika orodha na kuichapisha orodha hiyo yenye majina ya watu wote

walioruhusiwa na Chama kwenye angalau gazeti moja linalopatikana kote nchini Kenya, na tena nakala za orodha hiyo zitapelekwa kwa Afisi ya Rais, Msimamizi Mkuu wa Uchaguzi, Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na wasimamizi wote wa uchaguzi.

12. Orodha itakayochapishwa chini ya kanuni nambari 11 itakuwa tayari kukaguliwa kwenye ofisi za wasimamizi uchaguzi na mtu ye yote mwenye haja ya kuikagua chini ya utaratibu wa uteuzi wa Chama, kwa muda wa siku tatu baada ya kuchapishwa.

13. Mtu ye yote anayeona kwamba jina lake limesahuliwa kuandikwa, au limeondolewa kwa makosa, au limeondolewa kwa njia isio sawa kutoka kwenye orodha hiyo, atakuwa na haki ya kupeleka malalamiko au kukata rufani kwa Rais wa Chama mnamo muda wa siku nne baada ya kumalizika wakati wa ukaguzi wa orodha hiyo.

#### **Sehemu ya Nne: Kujipeleka kwa Wagombea-Uchaguzi kwa Wasimamizi wa Uchaguzi**

14. Kwa kutegemea siku na wakati au nyakati zitakazotangazwa na Rais wa Chama, wagombea-uchaguzi wote itawabidi wafike mbele ya wasimamizi wa uchaguzi wao wanaohusika wakiwa na:

- (a) Kitambulisho cha taifa.
- (b) Shahada ya uanachama wa maisha ya Chama.
- (c) Kadi iliyoandikishwa ya kupigia kura.
- (d) Malipo ambayo hayatarudishwa ya kudhaminiwa Chamani ya shilingi za Kenya 1,500 kwa ajili ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa na shilingi za Kenya 3,000 kwa ajili ya uchaguzi wa Bunge.

15. Mgombea-uchaguzi ye yote atakayeshindwa kufika katika siku na wakati na mahali palipotajwa kwa mujibu wa kanuni nambari 14, hataruhusiwa kushiriki katika utaratibu wa uteuzi.

16. Baada ya kumalizika shughuli ya kufika kwa wagombea-uchaguzi, kila msimamizi wa uchaguzi ataandika orodha ya wote waliofika mbele yake, na atapeleka nakala za orodha hiyo kwa Afisi ya Rais, Makao Makuu ya KANU, Msimamizi Mkuu wa

Uchaguzi, Mkuruguzi wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na wakuu wa vituo vya upigaji-kura walio chini ya mamlaka yake.

17. Wagombea-uchaguzi wote ambao majina yao yatapatikana kwenye orodha iliyoandikwa kwa kulingana na kanuni nambari 16 watapewa cheti mfano unaopatikana mwisho wa Kanuni hizi, cheti ambacho kitakuwa kimetiwa sahihi na msimamizi wa uchaguzi kinachothibitisha kwamba wametimiza mahitaji yote ili yapelekwe kwa wakuu wa vituo vya upigaji-kura kwa ajili ya uteuzi.

### **Sehemu ya Tano: Kujipeleka kwa Wagombea-Uchaguzi kwa Wakuu wa Vituo vya Upigaji-Kura**

18. Kwa uchache, kabla ya siku 21, kabla ya uchaguzi wote uliotajwa kwenye kanuni nambari 3 kutokea, Rais wa Chama ndiye atakayechagua siku ambayo wagombea-uchaguzi ambao majina yao yamo kwenye regista, na kujipeleka mbele ya wakuu wa vituo vya upigaji-kura kwa ajili ya uteuzi.

19. Kila mgombea-uchaguzi ni lazima kuhudhiria yeye mwenyewe au kumpeleka ajenti wake kwenye kila kituo cha upigaji-kura kilichotangazwa katika mawakilisho au wadi ambako angetaka kugombea uchaguzi.

20. Kila mgombea-uchaguzi au ajenti wake ni lazima kufikisha hati au nyaraka zifuatazo kwa mkuu anayehusika wa kituo cha upigaji-kura:

- (a) Cheti au nakala ya cheti kilichotolewa na msimamizi wa uchaguzi chini ya kanuni nambari 17.
- (b) Kadi halisi ya uanachama wa Chama.
- (c) Kitambulisho cha Taifa.
- (d) Kadi ya upigaji-kura iliyoandikishwa ikiwa na jina la mawakilisho au wadi inayohusika.

### **Sehemu ya Sita: Uwezo wa Wapigaji-Kura na njia ya Upigaji-Kura**

21. Wanachama wote wa KANU waliokwisha lipa ada zao kwa ukamilifu, na ambao hawakusimamishwa uanachama wao kutoka kwenye Chama, au wale ambao hawajazuiliwa kupiga kura chini

ya ibara nambari 7 na nambari 265, watakuwa na haki ya kuonyesha mtu wanayempigia kura kwa kupanga mstari nyuma ya mgombea-uchaguzi au nyuma ya ajenti wake.

22. Kwenye kila kituo cha uchaguzi, kanuni zifuatazo zita-fuatwa:

- (a) Vituo vya uchaguzi vitaandikwa majina wazi wazi na mkuu wa kituo cha upigaji-kura.
- (b) Upigaji-kura kwa wagombea uchaguzi wa Bunge utanza saa sita mchana siku itakayotangazwa chini ya kanuni nambari 18, na utaendelea mpaka wakati ambapo mkuu wa kituo cha upigaji-kura amekwisha zishughulikia kura zote kwa mujibu wa Sehemu ya Saba ya Kanuni hizi.
- (c) Upigaji-kura wa wagombea-uchaguzi wa Serikali za Mitaa utanza mara tu baada ya kura za wagombea-uchaguzi wa Bunge kumaliza kushughulikiwa, na kuendelea hadi mkuu wa kituo cha upigaji-kura atakapokwisha kuzishughulikia kura zote kwa mujibu wa Sehemu ya Saba ya Kanuni hizi.
- (d) Hapana kampeni yo yote itakayoruhusiwa kwenye eneo lililo karibu na kituo cha uchaguzi.
- (e) Isipokwa msimamizi wa uchaguzi, mkuu wa kituo cha uchaguzi, maafisa wa uchaguzi na maajenti waliokubaliwa, watu ambao hawakuandikishwa kama wapigaji-kura kwenye kituo cha upigaji-kura hawataruhusiwa kuingia au kupiga kura kwenye kituo hicho, na watu kama hao hawataruhusiwa kubaki kwenye duara la yadi 100 ya kituo hicho cha upigaji-kura.
- (f) Maajenti wote ambao orodha yao atapewa mkuu wa kituo cha upigaji-kura watabeba picha nyeupe na nyeusi (isiyokuwa ya rangi yo yote) yenye upana na urefu wa inchi 16 kwa inchi 24 ya mgombea-uchaguzi wanayemwakilisha.
- (g) Wapigaji-kura wote watazibeba kadi zao za uanachama wa KANU kwa namna ambayo itaonyesha stampu za Chama zilizokwisha bandikwa.
- (h) Wapigaji-kura ni lazima wawe watulivu na kusimama kwenye mstari wakati wote wa upigaji-kura.

- (i) Hapana mpigaji-kura atakayeruhusiwa baada ya kujiunga na mstari mmoja kuruka na kujiunga na mstari mwingine baada ya kuanza shughuli ya kuhesabu kura kwa mujibu wa Sehemu ya Nane ya Kanuni hizi.
- (j) Wapiga-kura wote watahitajika kujitambulisha kwa kuonyesha kadi halali ya upigaji-kura ya eneo hili.

### **Sehemu ya Saba: Kuhesabu Kura kwenye Vituo vya Upigaji-Kura**

23. Kuhesabu kwa kura kwenye kila kituo cha upigaji-kura kutafanywa kwa kuhesabu jumla ya wapigaji-kura waliosimama nyuma ya kila mgombea-uchaguzi au nyuma ya ajenti wake, kwenye kituo hicho.

24. Mkuu wa kituo cha upigaji-kura na maafisa wa uchaguzi chini yake watahakikisha kwamba kuhesabiwa kwa kura, kulingana na kanuni nambari 23, kunafanywa kwa njia ya utulivu, na kwa kuhakikisha idadi kuwa sahihi, na kwa njia ya usawa.

25. Pamoja na yale yaliyomo chini ya kanuni nambari 24, mkuu wa kituo cha upigaji-kura:

- (a) Atasikiliza na kuamua kwa haki malalamiko yote na mambo mengineyo yatakayoletwa kwake na wagombea-uchaguzi au maajenti wao.
- (b) Atahesabu kura kwa kuwahesabu wapigaji-kura kwenye kila mstari kwa sauti kubwa na kwa sauti inayosikika.
- (c) Ataandika idadi yote ya wapigaji-kura wa kila mstari kwenye cheti kitakachotiwa sahihi na mgombea-uchaguzi au ajenti wake.
- (d) Atampa kila mgombea-uchaguzi au ajenti wake nakala ya cheti kilichoelezwa chini ya kanuni nambari 25 (c).

26. Mara tu baada ya kura zote kuhesabiwa, kwa njia iliyoenezwa chini ya kanuni nambari 23 hadi kanuni nambari 25, wakuu wa vituo vya upigaji-kura watapeleka matokeo yote ya kila kituo cha upigaji-kura chini yao, matokeo hayo yakiwa yamefungwa mbele ya wagombea-uchaguzi wote au mbele ya maajenti wao, na kuyapeleka matokeo hayo kwa wasimamizi wa uchaguzi wanaohusika.

27. Iwapo mgombea-uchaguzi ye yote au ajenti wake atakataa kutia sahihi cheti cha matokeo au kupinga namna ambavyo matokeo hayo yalivyofungwa, mkuu wa kituo cha upigaji-kura ataliandika jambo hilo na sababu zilizotolewa kuhusiana na jambo hilo, na atalipeleka jambo hilo pamoja na matokeo ya uchaguzi kwa msimamizi wa uchaguzi.

28. Wapigaji-kura wote watatawanyika mara tu baada ya kuhesabiwa kwa kura kutakapomalizika, na kwa mujibu wa Sehemu hii.

### **Sehemu ya Nane: Kutangazwa kwa Matokeo na Uteuzi**

29. Atakapopokea matokeo kutoka kwa wakuu wote wa vituo vya upigaji-kura walio chini yake, msimamizi wa uchaguzi mbele ya wagombea uchaguzi wote au mbele ya maajenti wao, ataandika jumla ya kura zilizopigwa katika kila mawakilisho au wadi.

30. Msimamizi wa uchaguzi mara baada ya kufanya hivyo, atatangaza matokeo yaliyopatikana kutoka kila mawakilisho au wadi na kutangaza idadi kamili ya kura zote zilizopigwa na jumla ya kura alizopata kila mgombea-uchaguzi.

31. (i) Mgombea-uchaguzi ye yote ambaye amegombea uchaguzi bila kupingwa kwenye vituo vyote vya upigaji-kura katika mawakilisho au wadi yake na kwa njia iliyoelezwa kwenye Sehemu ya Tano ya Kanuni hizi au akapata zaidi ya kura 70 kwa mia (yaani asili mia sabini) ya kura zote zilizohesabiwa kwenye mawakilisho au wadi basi mgombea-uchaguzi huyo, bila ya uthibitisho wo wote mwingine, atatangazwa kuteuliwa na Chama kugombea uchaguzi kwenye mawakilisho au wadi na kwa mujibu wa masharti yaliyomo kwenye Sheria ya Uchaguzi wa Bunge na Uchaguzi wa Rais, ama kwenye Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

(ii) Mgombea uchaguzi ye yote ambaye—

(a) amepata kwa uchache 30 kwa mia (yaani asili mia thelathini) ya jumla ya kura zilizopigwa kwenye kila mawakilisho/wadi; au

- (b) amepata idadi kubwa zaidi ya wagombea-uchaguzi watatu waliopata idadi kubwa, na ambapo hapana mgombea-uchaguzi mwingine aliyetimiza masharti chini ya kanuni nambari (i), au kuwepo wagombea-uchaguzi chini ya watatu kwa mujibu wa kanuni nambari (ii) (a), iliyotajwa hapo juu,

basi mgombea-uchaguzi huyo, bila ya uthibitisho wo wote mwingine, atatangazwa kuteuliwa na Chama kugombea uchaguzi kwenye mawakilisho au wadi na kwa mujibu wa masharti yaliyomo kwenye Sheria ya Uchaguzi wa Bunge na Uchaguzi wa Rais, ama kwenye Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

- (iii) Mgombea-uchaguzi ye yote atakayeshindwa kuteuliwa kama ilivyoelezwa hapo juu, ikiwa hakutosheka na uamuzi wa msimamizi wa uchaguzi anaweza kukata rufani au kuwasilisha malalamiko yake kwa Rais wa Chama katika kipindi cha masaa 24 baada ya hapo, na Rais atakuwa na uwezo wa kubadili uamuzi huo, kama atakavyoona ni sawa.

#### **Sehemu ya Tisa: Fedha na Malipo**

32. Chama cha KANU kitalipa gharama zote za kuendesha shughuli za uteuzi, hizi zikiwa pamoja na gharama za uchapishaji, usimamizi, kupatikana kwa vifaa vyote na malipo ya maafisa wa uteuzi.

#### **Sehemu ya Kumi: Kwa Jumla**

33. Rais wa Chama anaweza kutoa amri za kuzifuata Kanuni hizi kwa njia bora zaidi, na amri zitakazotolewa chini ya Kanuni hii zinaweza kutoa nafasi ya—

- (a) kuchapishwa kwenye Gazeti la Serikali au kutoa ilani kuhusu vituo vya upigaji-kura;
- (b) kutoa maelezo zaidi ya kukata rufani au kuwasilisha malalamiko chini ya kanuni nambari 12;
- (c) mpango na njia ya upigaji-kura kwenye vituo vya upigaji-kura;
- (d) kutoa kiwango cha malipo ya maafisa wa uteuzi;
- (e) kutoa maelezo yo yote mengine yanayohusika na Kanuni hizi.

## CHETI CHA KUJIWASILISHA

(Chini ya Kanuni Nambari 17)

Cheti hiki kinathibitisha kwamba:

.....  
mwenye kitambulisho nambari .....

Nambari ya Shahada ya Uanachama wa Maisha wa Chama .....

.....  
Nambari ya Kadi Iliyoandikishwa ya Upigaji-kura .....

ametimiza mahitaji yote ya kujipeleka kwa wapigaji-kura kwa  
ajili ya kuteuliwa na Chama kwenye mawakilisho/wadi ya .....

.....  
Sahihi .....

*Msimamizi wa Uchaguzi*

Wilaya ya .....